**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MWANZA - MWANZACOHAS**

Simu : +255 282500239
Fax : 255 282500501
**Barua pepe:**principal@mwacohas.ac.tz

Chuo cha Afya na Sayansi
Shirikishi Mwanza
S.L.P 476, **MWANZA**
01.7.2026

**Jina ……………………………………….**
**…………………………………………….**
**…………………………………………….**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA HUDUMA YA UTOAJI WA DAWA ZA USINGIZI NA HUDUMA ZA WAGONJWA MAHUTUTI KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) imekuchagua kujiunga na mafunzo Huduma za Utoaji wada za usingizi **(NTA Level 7)** katika Chuo cha **-Afya na Sayansi Shirikishi Mwanza** Mafunzo haya ni ya miaka miwili (2).

Chuo kitafunguliwa tarehe **14 September, 2026** na unapaswa kuripoti chuoni kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 11.30 jioni. Endapo utashindwa kuripoti ndani ya wiki mbili (2) tangu chuo kufunguliwa nafasi yako itapotea na kujazwa na muombaji mwingine.

Ili kukamilisha usajili na kupokelewa chuoni unatakiwa kufanya yafuatayo: -

i) Kukamilisha malipo ya ada kama ilivyoainishwa katika majedwali ya gharama za mafunzo hapo chini (*Sehemu A*). Malipo haya yatafanyika kupitia benki na mitandao ya simu kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** utakayopewa kabla ya kuwasili chuoni. Ili kupata namba ya kumbukumbu ya malipo, tafadhali wasiliana na Mhasibu wa Chuo kupitia

namba ya simu **0755- 680-053 AU 0768-036-276.** Mwanafunzi ambaye hatalipa ada iliyoainishwa kwenye kipengele hicho hatapokelewa.

ii) Kujaza Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo utakayopewa ufikapo chuoni. Unakumbushwa kuzisoma na kuzielewa sheria zote kabla ya kusaini.

iii) Kujaza Fomu iliyoambatishwa hapo chini inayohusu Taarifa za Wazazi/Walezi wako/Ndugu wa karibu.

iv) Kununua vifaa vyote vilivyoainishwa katika sehemu B hapo chini vitakavyokuwezesha katika mafunzo yako uwapo chuoni. Hii ni pamoja na sare za chuo.

## SEHEMU A: MAELEKEZO YA MALIPO

Kila mwanafunzi atapaswa kulipa Jumla ya **Tsh 2,300,000.00 (Shilingi Milioni Mbili na Laki Tatu tu)** kwa mwaka. Fedha hizi zinajumuisha gharama za mafunzo zinazolipwa chuoni moja kwa moja na gharama zisizo za mafunzo zinazolipwa kwenye mamlaka na Taasisi nyingine za Serikali. **Fedha zikishalipwa hazirudishwi (non-refundable).**

Mchanganuo wa malipo ni kama ulivyoainishwa katika majedwali yafuatayo:

### I. Gharama zinazolipwa moja kwa moja Chuoni:

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatalipwa moja kwa moja chuoni kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number) itakayotolewa na MAMLAKA HUSIKA. Mwanafunzi anaweza kulipa malipo ya ada ya mwaka mzima kwa mara moja au kwa awamu mbili kama inavyoonekana katika mchanganuo ufuatao:

**Jedwali 1: Gharama zinazolipwa moja kwa moja Chuoni:**

| KIPENGELE | MALIPO MUHULA WA KWANZA | MALIPO MUHULA WA PILI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mafunzo | 750,000.00 | 750,000.00 | 1,500,000.00 |
| Mitihani ya Ndani | 75,000.00 | 75,000.00 | 150,000.00 |
| **Usajiri** | **30,000.00** | - | **30,000.00** |
| Michezo | 20,000.00 | - | 20,000.00 |
| Fedha ya Dharura | 20,000.00 | - | 20,000.00 |
| Mitihani ya Mwaka | - | 200,000.00 | 200,000.00 |
| **Mazoezi kwa vitendo na kitabu cha mazoezi** | **100,000.00** | - | **100,000.00** |
| Umoja wa wanafunzi | 30,000.00 | - | 30,000.00 |
| Transcripts | | 30,000.00 | 30,000.000 |
| Usimamizi wa field na tafiti | | 200,000.00 | 200,000.00 |
| **Kitambulisho** | **20,000.00** | | **20,000.00** |
| **JUMLA** | **1,045,000.00** | **1,255,000.00** | **2,300,000.00** |

**NB: 1**. **Malipo ya Usajiri, Mazoezi kwa vitendo, kitabu cha mazoezi** na **Kitambulisho** ( jumla 150,000) utatakiwa kulipa mara kabla yakufika chuoni ili kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho pamoja na viafaa eneo la mafunzo kwa vitendo (piga simu ili upatiwe control number **0755- 680-053 AU 0768-036-276**

**2.** Malipo tajwa katika Jedwali namba 1, yanapaswa kufanyika kila mwaka wa masomo. Ada ya muhula wa kwanza italipwa yote mara tu unapowasili chuoni na ya muhula wa pili italipwa ndani ya siku 14 baada ya kuanza muhula wa pili.

**3. Wanafunzi ni lazima wafike na namba zao za NIDA . Chuo hakitahusika na ufuatiliaji wa NIDA.**

## II. Malipo ya Gharama za Mitihani ya Kitaifa, NACTVET na BIMA ya Afya (NHIF)

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatafanyika pia kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** itakayotolewa kwa kila mwanafunzi kupitia ofisi ya uhasibu ya chuo. Ikumbukwe pia kuwa malipo ya vipengele hivi yatafanyika mwanzoni mwa kila mwaka wa masomo.

**Jedwali 2: Malipo ya Gharama za NACTVET na BIMA ya Afya (NHIF)**

| KIPENGELE | KIWANGO CHA MALIPO |
|---|---|
| Gharama za Matibabu (kwa wasio na BIMA) | 50,400.00 |
| Malipo ya eneo analokwenda kufanyia field | 100,000.00 |
| NACTVET Quality Assurance | 20,000.00 |
| **JUMLA** | **170,400.00** |

**NB:**

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na kadi ya bima ya afya ili imsaidie akapohitaji huduma ya matibabu. Kulipia gharama za matibabu ni jukumu la mzazi. Ili mwanafunzi aweze kusaidiwa kupata kadi ya bima ya afya, mzazi ana wajibu wa kuhakikisha mwanafunzi huyo ana namba ya kitambulisho cha NIDA na kiwango cha fedha kinachotakiwa kwa ajili ya malipo hayo. Namba ya kitambulisho cha NIDA ni muhimu wakati wa usajili wa mwanafunzi katika Huduma za Bima ya Afya.

**Jedwari 3 : Fedha anazo takiwa kuja nazo mwanafunzi kutoka kwa mzazi/mlezi au mfadhili ni kama inavo onekana kwenye jedwali hapa chini.**

| | MATUMIZI | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| 1 | Matumizi binafsi mfano chakula, n.k | 15,000.00<br>(kila siku) |
| 2 | Malazi | 500,000.00 |
| 3 | Vitabu | 200,000.00 |
| 4 | Matumizi kipindi cha field | 250,000.00 |
| 6 | Kufanya tafiti | 500,000.00 |

**SEHEMU B: MAHITAJI YA MWANAFUNZI AWAPO CHUONI**

Yafuatayo ni mahitaji muhimu ambayo mzazi/mlezi utapaswa kumuandalia mwanafunzi kabla ya kufika chuoni.

**I. SARE ZENYE NEMBO YA CHUO:**

**Wanawake** : Sare utanunua ukiwa chuoni

**Wanaume**: Sare utanunua ukiwa chuoni

**NB: 1. Uniform zinapatikana maeneo ya chuo, hivyo ukifika utaonyeshwa mahali zinapopatikana**

**II. VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA MWANAFUNZI**

a) Kifaa cha kupimia mapigo ya moyo (Stethoscope)
b) Kifaa cha kupimia msukumo wa Damu (BP Machine)
c) Vifaa vya kuandikia kwa mfano madaftari, kalamu, rula n.k
d) Nguo na viatu vya michezo mbali mbali.
e) Mwanafunzi aje na computer mpakato (laptop) au simu yenye uwezo kama huo ili kurahisisha kujifunza

**III. VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA CHUO**

a) Picha nne (4) Passport size .

Karibu sana. Nakutakia utekelezaji mwema.

**MKUU WA CHUO**

**KIAMBATISHO I: Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo**

# CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MWANZA

**Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Wataalam**

**Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo** Kwa **Wanafunzi Waliochaguliwa Kujiunga na Masomo ya Afya**

**Jina la Chuo: ………………………………………………………………**

**Mwaka wa Masomo: ………………………………………………………..**

**Kozi: ………………………………………………………………………**

## SEHEMU A: SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

Sheria zote za chuo zimeelezwa kwenye kitabu cha ***Displinary code for students in Health Taining Institutions ya waka 2020*** ambayo utapewa ukifika chuoni na kusaini

## SEHEMU B: MWONGOZO WA MAVAZI

### 1. NGUO ZINAZORUHUSIWA CHUONI

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na pia ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa nguo zinazoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

***1.1 Kwa wasichana/wanawake***

a) Wavae sketi au gauni isiyo ya kubana, kitambaa kisichokuwa *transparent* na iwe ndefu ya kuvuka magoti akiwa amekaa
b) Kuvaa sare pamoja na vitambulisho wakati wote wa darasa, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo
c) Sare: Zilizoainishwa hapo juu
d) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)
e) Nguo safi na zilizopigwa pasi
f) Nguo za michezo na tisheti zilizochaguliwa na taasisi/ Serikali ya wanafunzi
g) Uvaaji wa soksi ndefu za aina moja zenye rangi nyeupe
h) Hijabu iwe ya rangi nyeupe na iwe fupi inayoingizwa kwenye sare

***1.2 Kwa wavulana/wanaume***

a) Kuvaa suruali ndefu zisizo za kubana (chupa) na kuchomekea na kufunga mkanda pamoja na kuvaa vitambulisho wakati wote wa darasani, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo
b) Sare: Kama ilivyoainishwa juu
c) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)
d) Nguo safi zilizopigwa pasi
e) Nguo zinazoendana na rangi iliyochaguliwa na taasisi/Baraza la taaluma
f) Nguo zenye mtindo wa kushona uliopitishwa na taasisi/Baraza la taaluma
g) Nguo za michezo na tisheti zilizochaguliwa na taasisi/ Serikali ya wanafunzi

h) Uvaaji wa soksi za aina moja zenye rangi nyeupe
i) Vest au T-Shirt inayovaliwa ndani ya shati iwe yenye rangi nyeupe

**1.3 Nguo za kujikinga na baridi zinazoruhusiwa kwa jinsia zote**

*a)* Sweta lenye rangi nyeupe lisilokuwa na urembo au maandishi yeyote.

## 2. NYWELE ZINAZORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na pia ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa mitindo ya nywele inayoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

***2.1 Kwa wasischana/wanawake***

a) Nywele fupi za asili za kuchania kitana
b) Nywele ndefu za asili zifungwe kwa vibanio kuelekea kisogoni ili sura ionekane na zisiachwe kuning'inia au kuongezea rasta
c) Nywele kusuka bila nywele za zakuninginia

***2.2 Kwa wavulana/ wanaume***

a) Nywele fupi za asili zinazolingana za kuchania kitana
b) Ndevu haziruhusiwi
c) Nywele za rasta haziruhusiwi

## 3. UREMBO UNAORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa aina ya urembo unaoruhusiwa ni kama ifuatavyo: a) Pete za ndoa b) Kucha fupi

c) Saa
d) Miwani kwa wenye matatizo ya macho
e) Kofia kwa wenye matatizo ya ngozi (Albino)
f) Kucha ndefu

## 4. VIATU VINAVYORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa viatu vinavyoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

a) Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni.
b) Viatu vya michezo wakati wa michezo

## 5. MAVAZI YASIYORUHUSIWA

### 5.1 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wasichana/ wanawake

a) Nguo zinazobana
b) Nguo (gauni/sketi) fupi zinazoacha magoti wazi
c) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua
d) Nguo zinazoonyesha maungo/ nguo za ndani (transparent)
e) Nguo zilizokunjamana (Hazikunyooshwa)
f) Nguo chafu (Hazikufuliwa)

g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo
h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
j) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za Serikali
k) Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi
l) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) kwenye sehemu ya magoti na mapajani
m) Kwenda na khanga/kitenge kwenye bwalo la chakula bila kuwa na nguo ya ndani
n) Kuvaa nguo za kulalia (night dress) kwenye makundi ya kusoma na kupita nazo kwenye mazingira ya chuo
o) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani
p) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma
q) T-shirt zenye picha za kutisha na maandishi yasiyo na staha

### 5.2 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wavulana/wanaume

a) Suruali aina ya kadeti au jeans kutumika kama sare (hata kama ni ya rangi ya khaki) b) Suruali za kubana (modo)
c) Shati la kubana (Slimfit)
d) Kuvaa suruali mlegezo (*Kata K*)
e) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua
f) Kufunga vifungo vichache vya shati ili kifua kionekane
g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo
h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
j) Suruali yoyote fupi au iliyoachwa bila kupindwa chini
k) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) kwenye sehemu ya magoti na mapajani
l) Kaptura ya aina yoyote
m) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani
n) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma
o) T-shirt zenye picha za kutisha na maandishi yasiyo na staha.

## 6. NYWELE ZISIZORUHUSIWA

a) Nywele chafu ambazo hazikutengenezwa vizuri
b) Nywele bandia au zilizopakwa rangi

c) Kufuga nywele ndefu kwa wavulana/wanaume

d) Kusuka rasta ndefu au mtindo wowote wa nywele za kuning'inia

e) Unyoaji nywele mitindo isiyofaa k.m *kiduku, pank*, *zungu la unga* (kipara) f) Kufuga ndevu

g) Kunyoa ndevu kwa mitindo isiyofaa k.m mzuzu, *timberland au kufuga ndevu* n.k

**7. UREMBO USIORUHUSIWA**

a) Hereni, Bangili, Mikufu, Pete ambazo si za ndoa pamoja na manukato yenye harufu kali b) Kunyoa nyusi na kupaka wanja c) Kupaka rangi za midomo

d) Kufuga kucha ndefu na upakaji rangi kwenye kucha

e) Uvaaji wa kucha bandia

f) Meno ya urembo wa dhahabu hayaruhusiwi

**8. VIATU VISIVYORUHUSIWA**

a) Kandambili pamoja na makobazi

b) Viatu vya michezo pamoja na raba (isipokuwa wakati wa shughuli maalum za michezo)

c) Viatu vya rangi isiyopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

d) Kuvaa viatu bila socks

e) Viatu vya mchuchumio

f) Viatu vya kisigino vyenye kutoa sauti kwenye sakafu

g) Kufuga ndevu

**ANGALIZO:** Uvunjaji wa taratibu zilizoainishwa hapa juu unaendana na adhabu, ambazo zimeelekezwa katika kitabu cha maadili ya wanafunzi walioko katika vyuo vya afya kilichotolewa, ***na wizara ya afya mwaka 2019 (Disciplinary Code for Students in Health Training Institutions Revised 2019)***

**SEHEMU C: UTHIBITISHO**

Mimi........................................................................niliyechaguliwa kujiunga na masomo ya Afya kwa kada ya……………………………………. Ngazi ya …………………………………………….. nathibitisha kuzisoma na kuzielewa Sheria na Taratibu za Chuo pamoja na Mwongozo wa Mavazi niwapo chuoni.

Hivyo nathibitisha kuwa nitakuwa tayari kuzifuata kwa kipindi chote nitakachokuwa hapa chuoni na nakubali kuchukuliwa hatua za kinidhamu endapo nitathibitika kukiuka taratatibu hizo.

**Jina la Mwanafunzi**: ………………………………………………………………

Sahihi: ……………………………………………………………………………….

Tarehe: ………………………………………………………………………………

Jina la Mkuu wa taasisi ulitotoka/mlezi: …………………………………………………………………

Sahihi ya mkuu wa taasisi: ……………………………………………………………………….

Tarehe: …………………………  Muhuri …………………………………………..

Imepokelewa na kushuhudiwa na:

**Jina la Mkuu wa Chuo**: ……………………………………………………………

Sahihi:  ……………………………………………………………………………..

Tarehe: ……………………………………………  Muhuri……………………

**KIAMBATISHO II: Fomu ya Matibabu**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF HEALTH**

**MEDICAL EXAMINATION FORM FOR STUDENTS JOINING ALLIED HEALTH TRAINING INSTITUTIONS**

**NAME OF THE INSTITUTION: …………………………………………………………**

**PROGRAMME: ……………………………………………………………………….**

**YEAR OF STUDY: ……………………………………………………………………**

**PART A: STUDENT'S PARTICULARS**

STUDENT'S FULL NAME: ………………………………………………………………..

DATE OF BIRTH: ……………………………………………………………………….

SEX: (Male/Female)………………………MARITAL STATUS: ……………………………..

**PART B: STUDENT'S MEDICAL HISTORY**

Does the examinee have current history of any of the following? Indicate ***YES*** or ***NO***

Tuberculosis? ..............................

Epilepsy? .....................................

Sickle cell? ………………………

Asthmatic or with Allergic to something (*specify*)? …………..

Psychiatric? ……………………… Vision

impairment? ……………..

Hearing disorder? ……………….

Physical disability? ……………..

Any other significant medical condition/disorder? (*please specify*) …………………………

## PART C: PHYSICAL EXAMINATION

Height (cm): ……………………. Weight (kg): ………………….. BP (mmHg): ………………..

Any significant finding from systemic examinations (*please specify*):

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

## PART D: INVESTIGATIONS' FINDINGS

Please indicate any significant finding from the following Laboratory and Radiological tests

FBP: …………………………………….. Urinalysis: ………………………………………………

Random Blood Sugar (*provide the results*): ………………………… Blood group ……………….

Stool analysis: ………………………………

Any other relevant investigation performed (*please give brief findings*):

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

## PART E: CONCLUSION

I have examined Mr./Miss/Mrs… .....................................................................................and Consider that he/she is physically and mentally **fit/not fit** to be admitted to the college for studies.

| | | |
|---|---|---|
| …………………... | ...………… | …………………………………….. |
| Name | Signature | Date |

Qualification ………………………                Title ……………………………………….

Hospital's Name: ……………………………………………………………………………..

(*Official hospital's stamp*)

**<u>KIAMBATISHO III: Fomu ya Usajili</u>**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF HEALTH**

**INSTITUTION NAME: ……………………………………………………………….**

**STUDENT'S REGISTRATION FORM**

| **ADMISSION OFFICE** |
|---|

STUDENT NAME …………………………………………………………

DATE OF BIRTH ………………………………………………………….

NATIONALITY ………………………………………………………...

ADDRESS ……………………………………………………………………

SEX Male: ☐ Female: ☐

MARITAL STATUS ………………………………………………………

TELEPHONE NUMBER …………………………………………………

NACTVET REG NUMBER ………………………………………………

PROGRAM ………………………………………………………………….

NTA LEVEL ………………………………………………………………

REMARKS FROM NACTVET SYSTEM Available: ☐ Not Available: ☐

*If **Not Available**, state why?*

……………………………………………………………………………………………..

ADMISSION OFFICER'S SIGNATURE ……………………………………………

## TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

Passport size

**NDUGU WA KWANZA**

JINA KAMILI (MATATU) …………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI……………. ……………………………………

ANUANI YA POSTA: ………………………………………………………………

MTAA: ……………………………KATA: ………………...WILAYA: ………….

MKOA: …………………………………………NAMBA YA SIMU: ……………………

BARUA PEPE: ………………………………………….

**NDUGU WA PILI**

JINA KAMILI (MATATU) ……………………………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI……………. …………………………………………………...

ANUANI YA POSTA: ……………………………………………………………………………

MTAA: ……………………………KATA: ………………...WILAYA: …………………...

MKOA: …………………………………………NAMBA YA SIMU: ……………………

BARUA PEPE: ………………………………………….

Nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi na kweli tupu.

JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI/MWENZA/MKUU WA TAASISI ALIYOTOKA

………………………..…………………………………………….

SIMU YAKE…………………………………………………………

SAHIHI: ……………………………………………. TAREHE:…………………………………………….

Imesainiwa mbele ya (Ijazwe na Mtendaji wa Kata/mtaa/Kijiji)

JINA KAMILI ……………………………………………CHEO: ……………………………………..

ANUANI YA POSTA: ………………...……………………………………………………………..

MTAA: ……………………………KATA: ………………..WILAYA: ……………………..

MKOA: …………………………………………NAMBA YA SIMU: ………………………..

SAHIHI: ………………………………. MUHURI WA OFISI: ………………………………

TAREHE: ……………………………………………………….

## ACCOUNTANT'S OFFICE (*Payment of School Fees*)

TOTAL AMOUNT PAID ……………………………………………..

TOTAL AMOUNT NOT PAID …..…………………………………………..

REASON FOR AMOUNT NOT PAID ……………………………………………..

………………………………………..………………………………………….

………………………………………..………………………………………….

PAID SMESTER II EXAMINATION FEES? **YES** ☐ **NO** ☐

ACCOUNTANT'S SIGNATURE ……………………………………………..

STUDENT'S SIGNATURE ……………………………………………..

## PATRON / MATRON OFFICE (*if accommodation offered*)

HOSTEL NAME / BLOCK ……………………………………………..

ASSIGNED ROOM NUMBER ……………………………………………..

STUDENT'S DISABILITY (*Briefly describe in case of any disability*)

………………………………………..……………………………………………..

………………………………………..……………………………………………..

………………………………………..……………………………………………..

PATRON / MATRON SIGNATURE ……………………………………………..

## STUDENT'S DECLARATION

I..........................................................................declares that all the information provided are correct to the best of my knowledge and shall be held responsible in case of wrong information.

STUDENT'S SIGNATURE ……………………………………………..

DATE ……………………………………………..

**WIZARA YA AFYA**

**KIAMBATISHO NA. IV: FOMU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. **Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi**

Mimi Bw./Bi/ ............................................................................................... ambaye ni /Mkuu wa Taasisi, mzazi/mlezi wa Bw./Bi……………………………………………………….…nakiri kupokea maelekezo ya Wizara/Chuo. Ninaahidi kumsimamia atekeleze maelekezo yote ikiwa ni pamoja na kulipa ada kwa ukamilifu ili aweze kupokelewa chuoni na kuanza masomo ndani ya muda uliopangwa. Pia ninaahidi kushirikiana na uongozi wa chuo kuhakikisha mwanafunzi huyu anasoma kwa bidii na kuonyesha nidhamu wakati wote wa mafunzo.

2. **Taarifa ya Mtendaji wa kata**

**Jina la Afisa Mtendaji wa Kata:** ………………..……………………………..………………..

**Jina la kata:** …………………..…………………..………………………………..

**Anuani :** ……………………………………………………………………………….

**Namba za simu:** ……………………………………………………………………………….

**Barua pepe:** ……………………………………………………………………………….

**Saini**: ……………………………………………………………………………….

Muhuri wa ofisi